جمهورية مصر العربية
وزارة الأوقاف

٦ شعبان ١٤٤٠ هـ
١٢ إبريل ٢٠١٩م



# Masharti na Maadili ya Masoko.

Prof.Ayman Al-asar

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu: {Ole wao hao wapunjao! Ambao wanapo jipimia kwa watu hudai watimiziwe. Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza. Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa. Katika Siku iliyo kuu. Siku watapo msimamia watu Mola Mlezi wa walimwengu wote}. Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote. Na mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Ama bado,Na baada ya utangulizi huu.

Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amewawekea waja wake utaratibu wa kuuza na kununua ili kulifikia lengo na kwa ajili ya mahitaji ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

**{وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا}،**

{Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameiharimisha riba}.

Na tangu kale imezoeleka kwa watu kuandaa masoko ambayo wanakishiana mahitaji yao ya kuuza na kununua na kuyafikia masilahi yao, na kupitia masoko hayo, na zimekuja aya za Quran tukufu ili zibainishe alama kati ya alama za ubinadamu, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**{وَما أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ}**

{Na hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakenda masokoni.}

Na Qurani ikasimulia kauli ya Washrikina kuhusu Mtume( S.A.W )aliposema:

{وَقَالُوا مَالِ هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ}،

{Na wakasema: Ana nini Mtume huyu? Anakula chakula, na anatembea masokoni!}.

Na katika Kisa cha Watu wa Pangoni"Ahlulkahfi", Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

{فَابْعَثُوا أَحَدَكُمْ بِوَرِقِكُمْ هَذِهِ إِلَى الْمَدِينَةِ فَلْيَنْظُرْ أَيُّهَا أَزْكَى طَعَامًا فَلْيَأْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِنْهُ}.

{Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu ende mjini, akatazame chakula chake kipi kilicho bora kabisa akuleteeni cha kukila.}.

Na katika jambo lisilokuwa na Shaka yoyote ndani yake ni kwamba hali za Masoko ni moja ya mambo yanayotekelezwa kivitendo katika Uislamu na iwapo utataka kujia athari za ibada katika mienendo ya watu basi nenda Sokoni, na ukitaka kutoa hukumu ya ukweli wa kufuata Dini au kuwa kwake mtu ni mfuasi wa Dini basi unapaswa kuifuatiliaienendo ya mtu katika

kuamiliana kwake kwa kuuza na kununua, na kwa hivyo, pale mtu mmoja alipotoa ushahidi kwa Bwana wetu Omar R.A, naye akamwambia: Mimi sikujui na wala haikudhuru wewe mimi kutokukujua, hebu mlete mtu anaekujua. Mtu mmoja miongoni mwa waliokuwapo akasema: Mimi ninamjua. Omar akasema: wewe unamjua kwa lipi? Yule mtu akasema: Ninamjua kwa Uadilifu na Fadhila. Omar akasema: kwa hiyo huyu ni jirani yako wa karibu ambaye wewe unaujua usiku wake na mchana wake na unaijua njia yake ya kutokea na ya kuingilia? Akasema hapana. Kwa hiyo kwa mtangamano wako kwa dinari na dirhamu ndivyo vinavyotumika kama dalili unyenyekevu? Akasema hapana. Omar akasema: je ni rafiki yako safarini ambae inapatikana dalili ya tabia njema? Akasema hapana. Omar akasema: kwa hiyo weye humjui huyu. Kisha akasema: Njoo na mtu anaekujua.

Kwa hiyo miamala ya kuuza na kununua hudhihirisha ukweli wa Dini ya mja na uongo wake au kujipamba pamba kwa, na kupitia miamala hiyo hudhihirika mwonekano wa kufuata Dini, au ufuasi wa kweli wa Dini kiutekelezaji, na ni wangapi katika

wale waliomtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ndimi zao ili wawajengee watu fikra ya kuwa wanafuata Dini ili, lakini kumbe wawadanganye wengine. Na wao wako mbali na kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu kiuhalisia! Na ni wangapi wenye kujificha nyuma ya sura ya wafuasi wa Dini kwa ajili ya kujionesha kwa watu na kutaka kujulikana, na kama njia ya kujichumia mali, au kwa ajili ya kutangaza bidhaa zake mtu, na wakifanya makusudi jinsi watu wanavyoipenda Dini, na imani yao kwa watu wenye Dini.

Na miongoni mwa sura danganyifu pia: ni kuviita vitu kwa majina yasiyoendana na vitu, kwa lengo la kuwapotosha watu kwa kujifanya mfuasi wa Dini au kuitumia kibiashara, pamoja na kwamba ukweli wa mambo ni kinyume kabisa na hivyo, ili tu mtu ajipatie Chumo na mali hali ya kuwa kwa kitendo chake hicho anaudhuru Uislamu na kujenga sura mbaya katika nafsi za watu. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَمِنَ النَّاسِ مَن يُعْجِبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشْهِدُ اللَّهَ عَلَى مَا فِي قَلْبِهِ وَهُوَ أَلَدُّ الْخِصَامِ * وَإِذَا تَوَلَّى سَعَى فِي الْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْفَسَادَ}.

Kwa maana ya Kiswahili:{Na katika watu yupo yule ambaye maneno yake kwa maisha ya kidunia hukufurahisha; naye humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ndiye mkubwa wa ukhasimu. Na anapo tawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi.} Na Mwenyezi Mungu anasema pia:

قال تعالى : {يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ}،

Kwa maana :{Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli.}.

Na katika Maadili ya Soko: Ni wao kutopunja ujazo au Mizani. Na kinachokusudiwa hapa katika upunjaji ni kutotimiza kwao kipimo au ujazo, na kupunja au kutia hasara wakati wa kupima,

akatumia vifaa vinsvyofanana na vipimo vya kweli katika vipimo na vigezo wanavyovitumia watu.Na Mwenyezi Mungu anasema pia juu ya uadilifu wa kipimo na mizani:

{وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلا}

Kwa maana:

{Na timizeni kipimo mpimapo. Na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na hatimaye ndio bora}.Na anasema pia:

{وَيْلٌ لِلْمُطَفِّفِينَ* الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ * وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ}.

Kwa maana:{Ole wao wale wapunjao. Ambao wanapo jipimia kwa watu hudai watimiziwe. Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza} .

Na Nabii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Shuaib aliwaonya watu wake kuwapunja watu vitu vyao na kupunguza ujazo katika

vipimo vyao na mizani, kama inavyosimulia Qurani tukufu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**{وَإِلَى مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا قَالَ يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ قَدْ جَاءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ فَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ}.**

{Na kwa watu wa Madyana tulimtuma ndugu yao Shua'ib. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Hamna mungu mwengine isipo kuwa Yeye. Imekwisha kufikieni hoja wazi kutoka kwa Mola Mlezi wenu. Basi timizeni sawasawa vipimo na mizani, wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika nchi, baada ya kuwa imekwisha tengenea. Hivi ndivyo bora kwenu ikiwa nyinyi ni Waumini.}.

Na katika maadili ya Soko: Ni kutozikiuka haki za wengine, na kwa ajili hiyo, Mtume( S.A.W) amezuia mtu kuuza dhidi ya nduguye akasema: Asiuze miongoni mwenu yoyote dhidi ya mauzo ya nduguye.

Na katika Mapokezi mengine: Asiuze mtu dhidi ya bei ya Ndugu yake wala asimvurugie nduguye thamani ya bidhaa yake,

mpaka amruhusu au aache. Na haya ni miongoni mwa Maadili ya juu ya kuuza na kununua, kwa hiyo mchuuzi asitake kumwongezea mnunuzi bidhaa (ili anunue zaidi), lakini pia asiitie kasoro bidhaa ya nduguye ili auze yake, bali avumilie mpaka aiuze.

Na miongoni mwa sura za uvunjifu wa haki za wengine ni ulanguzi au kuhodhi soko, ambako kunapatikana kwa kuchezea vyakula vya watu na kuidhuru nchi na watu. Na Mtume wetu anasema: Hakuna mtu yoyote anayehodhi soko isipokuwa mtu aliyefanya makosa.

Kwa hiyo, mtu anaehodhi bidhaa ni mtu aliyeelemewa na umimi na akachagua kujipendelea badala ya kuwapendelea wengine na akasahau kuwa faida iliyozidi ambayo anaipata na anajipatia kwa njia ya ulanguzi na kwa kutumia kwake mali ya haramu, mali hiyo ya Haramu ni yenye kuangamiza hapa Duniani na kesho Akhera, ambapo anasema Mtume S.A.W:

Mtu yoyote atakaehodhi kwa Waislamu chakula chao, Mwenyezi Mungu Mtukufu atampiga kwa maradhi ya ukoma na kufilisika.

Na anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakayehodhi soko la chakula kwa siku arubaini basi atakuwa amejitenga na Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mwenyezi Mungu Mtukufu amejitenga naye, na wale wenye uwezo wa chakula, wameakiwa na mtu mwenye njaa, basi watakuwa wamejitenga na hifadhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kama ambavyo sisi tunasisitiza kwamba kuyachunga Masoko ni katika majukumu makuu ya nchi na kwamba ni lazima kushirikiana na vyombo vyote vinavyohusika, ili kuzuia kila aina ya makosa ya udanganyifu na ulanguzi pamoja na kumtumia mlaji, kwani kuyafyeka makosa haya mabaya kutachangia kwa nguvu kuleta usalama wa kijamii, na kutachangia kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya kiuchumi na kupambanuka pamoja na kufanya vizuri kiutendaji ndani na nje ya nchi. Ama kwa upande wa udanganyifu, mlango wake ni mpana mno kati ya milango ya ufisadi na uporomoshaaji wa uchumi wa nchi mbalimbali.

Kama ambavyo sisi tunasisitiza kwamba usimamizi wa masoko na uchungaji wake ni amana kubwa na ni jukumu zito mikononi

mwa kila aliyepewa kazi miongoni mwa kazi mbalimbali za masoko, na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mwenye kumuuliza kila mtu kile alichokalifishwa, je alikilinda au alikipoteza?

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

* * *

**Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya wa Mwisho katika Mitume, na Wajumbe wake, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote.**

Tunazungumza katika hotuba ya pili juu ya usalama wa binadamu katika vyakula na vinywaji vyake katika jamii.

Ndugu zangu Waislam.

Hakika usalama wa watu katika chakula chao, vinywaji vyao na mahitaji yao ni Suala la kijamii na la kibinadamu na linakuja kama kipaumbele cha kwanza katika haki za binadamu; kwani

haiwezekani kutafakari Maisha mazuri bila ya mtu kuwacna usalama wa chakula chake na dawa zake, na kwa hivyo ni lazima zikusanywe juhudi katika kupambana na aina zote za udanganyifu na kuhodhi masoko na hasa kwa yale mambo yanayohusiana na chakula pamoja na madawa.

Ni kwamba mfanyabiashara mwenye ufahamu wa Deni lake hudhirika athari ya ibada yake kutokana na Swala na swaumu na nyingine katika kuwa kwake mkweli na mwaminifu, kwani huwenda mfungaji akawa hana kitu katika swaumu yake isipokuwa njaa na kiu tu, na huwenda mfanya ibada za usiku akawa hana kitu katika kukesha kwake kwa ibada isipokuwa tabu na mkesha tu, na Mtume S.A.W ameelezea Daraja la juu la mfanyabiashara mkweli na mwaminifu na nafasi yake ya juu akasema: Tajiri mkweli na mwaminifu yuko pamoja na Manabii na wasema kweli pamoja na Mashahidi. Na anasema Mtume S.A.W: Hakika chumo bora kuliko yote ni la wafanyabiashara ambao wanapozungumza huwa hawasemi uongo, na wanapoaminiwa huwa hawafanyi hiana, na wanapoahidi hawaendi kinyume na ahadi zao, na wanaponunua

hawadhulumu, na wanapouza hawapunji na wanapokuwa na deni hawacheleweshi na wanapodai hawaweki uzito.
Mtume S.A.W anasema pia kwamba: Mfanyabiashara Mkweli atakuwa katika kivuli cha Arshi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, siku ambayo hapatakuwapo kivuli chochote isipokuwa kivuli hicho. Na amesema Mtume S.A.W: Mfanyabiashara mkweli atakuwa chini ya kivuli cha Arshi siku ya Kiama.
Ni kwa kiasi gani sisi tunajitahidi kushirikiana pamoja kwa ajili ya maslahi yote ya Umma ambayo sote tunavuna matunda yake, kwani kila mmoja atamwangalia ndugu yake kwa jicho la huruma na akampendelea kile anachokipendelea kwa nafsi yake, na kwa hivyo muuzaji akawa mkweli kwa mnunuzi kama vile yeye ndiye mnunuzi, na mnunuzi naye akawa mkweli kwa mchuuzi kama vile yeye ni mchuuzi, . Na hii ni dalili ya Imani, ambapo Mtume S.A.W anasema: Haamini yoyote kati yenu mpaka ampendelee nduguye kile anachokipendelea kwa nafsi yake.
Ewe Mola wetu, tunakuomba ututajirishe kwa halali kwako na utuepushe na kila ulichokiharamisha, na utukinge kwa fadhila

zako na yoyote asiyekuwa Wewe.Na dua yetu ya mwisho ni Al-Hamdulillahi Rabi Al-Alameen .